

Kabla ya Matibabu



Baada ya Matibabu

Uhusiano kati ya kifua kikuu na ukoma

Magonjwa ya kifua kikuu na ukoma husababishwa na vimelea ina ya bakteria wa jamii ya "mycobacteria" na maambukizo ni kwa njia ya hewa kutoka kwa mgonjwa kwenda kwa mtu mwingine.

Vimelea vya kifua kikuu huzaliana katika mapafu na kuenea katika viungo vingine, na vile vya ukoma hushambulia mishipa ya neva na ngozi. Ukubwa wa madhara ya kifua kikuu na ukoma hutegemea kiwango cha kinga mwilini.




Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,
Wazee na Watoto



Kwa maelezo zaidi wasiliana na
mtoa huduma wa / za Afya aliye karibu nawe.

Kimetolewa na:
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,
Wazee na Watoto


kupitia
Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua
Kikuu na Ukoma
S.L.P. 9083, Dar es Salaam, Tanzania.
Barua pepe: info@moh.go.tz,
Tovuti: www.ntlp.go.tz,
Toleo la 2016



ATHARI ZA UGONJWA

KIFUA KIKUU / UKOMA

ATHARI ZA UGONJWA WA UKOMA



Athari za Ukoma hutokea kwa mtu aliyethirika na ugonjwa wa ukoma. Athari ni matokeo ya kinga ya mwili kukabiliana na vimela vya ukoma. Hii haina maana ya kuwa ugonjwa unazidi au kwamba matibahu hayafai.

Athari inaweza kutokea kabla, wakati au baada ya matibabu ya ukoma

Umuhimu wa kujua athari za ugonjwa wa ukoma

Athari za ukoma ndio sababu kuu ya uharibifu wa mishipa ya fahamu na kusababisha ulemavu kwa mtu aliyegua au anayeugua ukoma. Hivyo ni muhimu kuzitambua dalili za athari mapema na kuchukua hatua zinazostahili ili kutibu athari hizo na kuzuia ulemavu.

Dalili za Athari za Ukoma

- Mabaka ya mwili yaliyopo yanakuwa mekundu na yanavimba
- Kujitokeza kwa vinundu vyekundu vinavyouma.
- Macho kuwa mekundu na kutoa machozi
- Mishipa ya fahamu kuuma na kuvimba.
- Kuathiriwa kwa mishipa ya ahamu ambazo dalili zake ni kama vile kupoteza hisia, kuchomachoma kwa viganja vya mikono na nyayo za miguu na udhaifu wa misuli katika viungo hivyo.
- Homa na kunyong'onyea mwili
- Mikono na miguu inaweza kuvimba



Hatua za kuchukua mtu akipata dalili za athari za ugonjwa wa ukoma

- Ukiona dalili moja au zaidi kati ya hizo zilizotajwa hapo juu wahi kwenye kiuto cha tiba kwa uchunguzi
- Tumia dawa utakazopewa hadi mwisho kulingana na maelekezo
- Kama uko kwenye tiba ya ukoma, endelea na tiba hiyo pamoja na tiba ya athari za ukoma

Athari za Ukoma inahitaji tiba kwa dawa maalumu kwa sababu inaweza kuleta ulemavu wa kudumu.